TANGAZO LA SERIKALI NA.109 la tarehe 24/2/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA KITWANA YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Eneo la Kitwana ya Mwaka 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi wa Manispaa ya Kahama.

*Tangazo la Serikali na.109 (linaendelea)*

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*
Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba A yenye majira – nukta 451107.26MS, 9585541.51KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Mashariki katika uelekeo wa KZ88°43'53.40"MS kwa umbali wa kilomita 5 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba B yenye majira - nukta 456165.61MS, 9585653.85KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Magharibi katika uelekeo wa KS3°31 27.24"MG kwa umbali wa kilomita
4.1 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba C yenye majira - nukta 455912.21MS, 9581545.45KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Magharibi katika uelekeo wa KZ73°23 25.09"MG kwa umbali wa kilomita 5 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba D yenye majira - nukta 451155.51MS, 9582964.26KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Magharibi katika elekeo wa KZ6°04'24.76"MG kwa umbali wa kilomita 2 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba E yenye majira - nukta 450919.09MS, 9585182.18KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Magharibi katika uelekeo wa KZ27°38'24.04"MG kwa umbali wa kilomita 0.42 hadi ulipoanzia."

Dodoma,
6 February, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*